# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

**HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO, MAONI NA USHAURI WA RIPOTI YA KAMATI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWA OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS, SERA URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

---

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema, ambavyo vimetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili tukufu la Mkutano wa Kumi na Moja tayari kutekeleza majukumu yetu ya msingi kwa nchi yetu kiujumla. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutukirimu neema zake ambazo kwa hakika sote ni wahitaji kwake.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kukushukuru na kukupongeza wewe pamoja na wasaidizi wako, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa umahiri mkubwa, namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekma na busara katika jukumu lenu la kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wetu katika chombo hiki muhimu kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** pongezi za pekee ziende kwa Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdalla na Uongozi mzima wa Ofisi ya makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi wakiongozwa na Waziri wao Mheshimiwa Hamza Hassan Juma kwa juhudi zao kubwa na mashirikiano wanayotuonesha katika utekelezaji wa kazi

zetu, Kamati inawataka wazidi kutekeleza na kusimamia majukumu yao kwa ubora na ufanisi zaidi ili kufikia hatua bora ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ikiwa ni Kamati mpya baada ya mabadiliko madogo yaliyofanywa na Mheshimiwa Spika kama Kanuni yetu ya Kudumu ya Baraza , kanuni ya 108(4) Toleo la 2020 inavyoelekeza kwa namna wanavyonipatia mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba sasa kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Abadalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Haji Shaaban Waziri | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Maryam Thani Juma | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *8.* | Nd. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *9.* | Nd. Shawana Mohammed Haji | Katibu |
| *10.* | Nd. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, kwa kutumia Kanuni ya 107(3) imepewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia; ambapo kazi hiyo ilifanywa vyema katika kipindi kilichopita na bado Kamati inazidi kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo hayo katika kazi zake za kila siku. Ripoti hiyo hujumuisha ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa wizara na Taasisi zake ambazo ilizifanyia kazi kwa mwaka wa fedha uliotangulia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kanuni ya *109(15)* ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la mwaka 2020 imetoa fursa ya lazima kwa kila Kamati kutayarisha ripoti ya mwaka itakayowasilishwa katika kikao cha mwezi wa Februari cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, kanuni ya *109(17)* ya Kanuni hizo za Baraza, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa mapendekezo hayo, Kamati inatakiwa kukaa na wizara/taasisi husika kujadili utekelezaji wa ripoti iliyowasilishwa Barazani katika mkutano husika.

**Mheshimiwa Spika**, katika Ripoti ya Kamati ambayo iliwasilishwa katika Mkutano wa Tisa wa Mwezi wa Februari, 2023 ilizihusisha Ofisi **tano (5)** ambazo ni:

- *(a)* Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;
- *(b)* Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais;
- *(c)* Ofisi ya Rais, Ikulu;
- *(d)* Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora; na
- *(e)* Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ.

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inaelezea muhtasari wa utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;

**UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO NA MAONI/USHAURI:**

**Mheshimiwa Spika**, jumla ya mapendekezo *15* yaliagizwa na Kamati katika mwaka wa fedha *2022/2023* kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi. Aidha, Kamati imefarijika sana na inatoa shukurani zake za dhati kwa Ofisi hii kwa jinsi walivyoweza kutekeleza

vyema maoni hayo hali inayoonesha ukomavu mkubwa katika utekelezaji wake pamoja na jitihada njema za kuleta maendeleo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya Ofisi kutekeleza vyema mapendekezo yaliyotolewa na Kamati, bado kuna wastani wa mapendekezo kadhaa ambayo Kamati imeona ni vyema kufanyiwa marekebisho na utekelezaji wake kuendelezwa kutokana na umuhimu wake kwa jamii. Hivyo, Kamati imeitaka Ofisi kufuatilia zaidi utekelezaji wa maoni na ushauri huo kwa kutoa maelekezo yafuatayo:

**Ushauri Nam. 1:**

> ***"Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kufuatilia na kusimamia kikamilifu taasisi za umma katika kutoa huduma zilizobora na kuhakikisha kuwa miongozo na ilani ya CCM inatekelezwa ipasavyo."***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kusimamia ipasavyo ushauri huu. Aidha, Kamati inazidi kusisitiza Ofisi kuzifuatilia baadhi ya taasisi za umma ambazo zinatoa huduma moja kwa moja katika jamii na zimekuwa zikilalamikiwa zaidi katika huduma zao. Kwa maana hiyo, zipo baadhi ya taasisi hasa kwa baadhi ya watendaji wake wanashindwa kutoa majibu kwa wakati wanapopelekewa barua za maombi au barua za utendaji wowote kuhusiana na taasisi zao hali inayopelekea kupungua kwa ufanisi wa kazi zao.

**Ushauri Nam. 7:**

> ***"Kamati kwa upekee inashuri itakapofika kuanza kazi kwa kituo cha Afya cha Uzi ajira za wafanyakazi wa kituo hicho kupitia vigezo vitakavyohitajika waangalie Zaidi wazawa wa kisiwa hiki.'***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitoa ushauri huu kutokana na hali ya kijografia ya eneo lenyewe ilivyo na kila mmoja anajua ugumu na uzito wa kufanya kazi katika mazingira ya visiwa vidogo vidogo. Hivyo, kuanza kazi kwa kituo cha Afya cha Uzi kutapelekea wananchi wa kisiwa hiki kutegemea huduma bora na safi ambazo zitapatikana kupitia uwepo wa Madaktari na wahudumu bora wa afya ndani ya masaa 24.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kufikia malengo hayo ni vyema taasisi husika kuzingatia ajira kwa wazawa au kufanya uhamisho kwa watumishi wazawa wenye sifa za kufanya kazi katika kituo hiki. Kupitia ushauri huu Kamati inasisitiza Ofisi ya Makamu wa Pili kwa kushirikiana na Wizara ya afya kupeleka vijana wazawa au kutoka maeneo ya karibu ambao watakuwa wazalendo katika kutoa huduma za kituo hiki.

**Ushauri Nam. 8:**

> ***"Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kutafuta eneo bora lenye kulingana na umuhimu wa majukumu yake katika ujenzi wa Ofisi za Wilaya hususan katika Wilaya ya Chake – Chake na Wilaya ya Mkoani."***

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto ya ukosefu wa ofisi za kudumu za Tume ya Uchaguzi katika ngazi za Wilaya hususan katika Wilaya zilizoainishwa kwenye ushauri wa hapo juu, Kamati bado haijaridhishwa na hali ya sasa ya mazingira ya ofisi za Wilaya yalivyo na hivyo, tunashauri Serikali kuweka nguvu maalumu katika utafutaji wa viwanja nakuandaa program za ujenzi wa ofisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, Kamati inashauri Tume kuangalia upya suala la kufanyika uchaguzi mdogo wa Majimbo na Wadi wakati viongozi wake wanapofariki huchukua muda mrefu bila ya kupangwa uchaguzi mwengine licha ya Sheria ya Uchaguzi Namba 4 ya Mwaka 2018 kutoa fursa ya kufanya hivyo lakini pia sheria hiyo hiyo

haikuzuia uchaguzi kufanyika mapema kutokana na wastani wa muda uliowekwa kisheria ambao ni miezi Minne hadi Kumi na Mbili.

**Ushauri Nam. 9:**

> ***"Tume ya Uchaguzi Zanzibar kufanya bidii katika kutafuta usafiri wake wenyewe na kutotegemea magari ya kuazima kwa kazi za Tume."***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati baada ya kupata majibu kwa ajili ya suala la usafiri wa Tume ya Uchaguzi, tumeridhishwa na namna ambavyo suala hili limepewa kipaumbele na hadi sasa Tume imeshapatiwa magari matatu na mengine Kumi yapo hatua za mwisho kuweza kupatikana ndani yam waka huu wa fedha. Jambo jema ni kwamba magari yaliyobakia yataenda kuondoa changamoto ya usafiri kwa ofsi za Wilaya kwa upande wa Unguja na Pemba.

**Ushauri Nam. 11:**

> ***"Serikali kuangalia kwa umuhimu wake suala la usafiri wa Kamati za Baraza ili kuendesha shughuli zake kwa ufanisi."***

**Mheshimiwa Spika,** katika kuangaliwa suala la usafiri kwa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi Kamati imeipongeza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuanza kutekeleza vyema agizo hili kwa kusaidia kupatiwa gari moja kwa ajili ya Mheshimiwa Spika. Hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha kwamba Ofisi ya Baraza la Wawakilishi inapatiwa gari kwa ajili ya shughuli za Kamati. Aidha, kamati imeshauri Ofisi kuandika upya kwa agizo hili na kuifanyiwa kazi kama ilivyoelekezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati inashauri kuhusu **Agizo Namba 12** na **Namba 15** kuhusu la Ujenzi wa jengo jipya la Ofisi na kumbi za Kamati kwa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kutekelezwa kama ilivyokusudiwa kwenye agizo hili kwani utekelezaji wake bado haujawa wenye kutia moyo.

**Ushauri Nam. 13:**

***"Katika maboresho ya Afisi ya Pemba, Kamati inashauri Baraza kusimamia kikamilifu matengenezo ya Ukumbi mkubwa wa Mikutano pamoja na Ofisi zake ili kuweka mazingira bora ya utendaji na shuguli zote za Serikali zinazofanyika hapo."***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaka Ofisi kuifanyia ukarabati Afisi ya Pemba hasa kwenye Ukumbi mkubwa wa mikutano kutokana na ukumbi huo kutumika katika shughuli mbali mbali za Serikali. Hata hivyo, Kamati imeelezwa kwamba Ukumbi wa Pemba kwasasa haupo kwenye umiliki wa Baraza na hivyo ni vigumu kuweza kuufanyia ukarabati mkubwa. Vile vile, ipo haja kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kufuatilia suala la umiliki wa Kumbi ya Idrisa Abdul Wakil na Ukumbi wa Afisi ya Pemba kuwa chini ya Ofisi ya Baraza la Wawakilishi.

**Ushauri Nam. 14:**

**"Afisi ya Baraza la Wawakilishi lizidishe kasi ya kutoa mafunzo kwa watendaji wake ili kupata watendaji wenye uzoefu na wanaendana na wakati na mazingira ya Mabunge."**

**Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji wa agizo hili, Kamati imeitaka Afisi ya Baraza la Wawakilishi kuwapatia watendaji wake mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi ili kuwajengea uwezo watendaji. Kamati inasisitiza Afisi kutekelza agizo hili kwa kuzingatia aina ya mafunzo inayohitajika kwa kilia Divisheni na kitengo. Sambamba na hilo, suala la mafunzo pia lipewe kipaumbele kwa watendaji wote wa ngazi za chini.

**Ushauri Nam. 15:**

***"Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kushirikiana na Wizara kuzidisha kasi ya kusimamia na kufuatilia haki na fursa za watedaji wa Baraza katika Nyanja zote za kimaslahi na mafunzo ili kufanya kazi kwa weledi na ufanisi zaidi."***

**Mheshimiwa Spika;** katika utekelezaji wa ushauri huu kwa upande wa afisi ya Baraza la Wawakilishi, Kamati inasisitiza kuendelezwa kwa juhudi za kuwapatia maslahi ya watendaji wa Baraza kufuatia kupindukia mwaka tangu kupatikana kwa muundo mpya wa Afisi na watendaji wote kuwekwa katika madaraja yao ya kiutumishi. Aidha, Kamati inashauri Ofisi kwa kushirikiana na Tume ya Utumshi wa Baraza kufuatilia kikamilifu maslahi ya watendaji wake ili kufahamu hatua iliyofikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuhitimisha, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yetu kuhusiana na utekelezaji wa maoni na ushauri tuliotoa katika ripoti ya mwaka 2022/2023 ambapo kwa ujumla utekelezaji wake umekuwa ukifanywa kwa kuzingatia malengo mahususi ya taasisi husika.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii tena kuishukuru Ofisi ya Makamu wa Pli wa Rais kwa mashirikiano yake inayoipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na pia niombe Ofisi hii kuzidisha mashirikiano hayo ili kuweza kufikia lengo la Serikali la kuleta maendeleo bora nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……………………

(Machano Othman Said),
Mwenyekiti,
Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,
**BARAZA LA WAWAKILISHI,**
**ZANZIBAR**